**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA HABARI MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI**

**SIKU YA POSTA DUNIANI TAREHE 9 OKTOBA, 2024**



***Mhe. Jerry William Silaa (Mb.)***

**UJUMBE KUTOKA KWA MHESHIMIWA JERRY WILLIAM SILAA (*Mb.*), WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI, JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA KATIKA MAADHIMISHO YA SIKU YA POSTA DUNIANI TAREHE 9 OKTOBA, 2024**

**KAULI MBIU:** ***"Miaka 150 ya Kuwezesha Mawasiliano na Kuboresha Maisha ya Watu Duniani".***

---

Ninayo furaha kubwa kuwasilisha ujumbe huu kwa wadau wa Sekta ya Posta na umma kwa ujumla, katika maadhimisho haya ya Miaka 150 ya Umoja wa Posta Duniani (UPU). Tanzania ikiwa ni miongoni mwa nchi Wanachama wa UPU, inaungana na nchi nyingine duniani kuadhimisha Siku ya Posta Duniani kwa kujenga

uelewa kuhusu nafasi ya Sekta ya Posta kwa jamii pamoja na mchango wake katika maendeleo ya kijamii na kiuchumi.

Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ilijiunga na umoja huu mwaka 1963 na imekuwa ikishiriki katika Taasisi mbalimbali za Kikanda na Kimataifa. Aidha, inaungana na UPU na Taasisi nyingine za Kikanda na Kimataifa kuadhimisha siku hii muhimu. Tanzania inayo furaha kuwa sehemu ya mtandao wa posta duniani kwani kupitia mtandao huo bidhaa na huduma zinaweza kufikishwa Duniani kote. Tunasherehekea maadhimisho ya Siku ya Posta Duniani ikiwa na mafanikio katika kuimarisha matumizi ya teknolojia ushirikiano na miongoni mwa wanachama katika kubadilishana barua, kujenga uwezo, msaada wa kiufundi kwa nchi zinazoendelea, na kuleta mageuzi ya Sekta ya Posta.

Kauli mbiu ya mwaka huu ni **"Miaka 150 ya Kuwezesha Mawasiliano na Kuboresha Maisha ya Watu Duniani".** Kauli mbiu hii inaeleza mchango wa Sekta ya Posta kwa kipindi cha karne moja na nusu iliyopita. Kauli mbiu hii pia inadhihirisha maendeleo ya makubwa yaliyofikiwa katika nyanja ya huduma za posta na mawasiliano kwa ujumla yaliyowezesha mabadiliko duniani.

Katika miaka hii 150 ya Sekta ya Posta duniani, ni muhimu tujikumbushe historia ya huduma za mawasiliano kabla ya mawasiliano ya kidijitali ambapo kutuma barua kwa njia ya posta ilikuwa ndiyo njia pekee ya mawasiliano. Endapo kulitokea ujumbe wa haraka basi telegramu ilitumika. Mawasiliano haya yalileta mapinduzi makubwa katika maeneo ya vijijini na mijini pia maeneo ambayo hayafikiwi na huduma kwa urahisi. Kwa umuhimu huu, huduma za posta bado zina nafasi muhimu sana katika kukuza uchumi na kuboresha jamii.

Nikiwa Waziri mwenye dhamana ya maendeleo ya Sekta ya Posta nchini, ninapongeza mafanikio yaliyofikiwa katika utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Posta ya mwaka 2003 pamoja na Sheria na Kanuni zinazosimamia Sekta ya Posta nchini. Kama nchi, kwa sasa tunaendelea na mapitio ya Sera ya Taifa ya Posta ya mwaka 2003 ili kukidhi matakwa ya kuwa na mazingira wezeshi kwa watoa huduma kwa kujumuisha matumizi ya teknolojia ili kuwezesha ubunifu, biashara mtandao na huduma za kidijitali kwa umma. Serikali imedhamiria kuhakikisha kuwa Sera inayofanyiwa mapitio inakidhi mahitaji na matumizi ya teknolojia katika kuboresha utoaji wa huduma. Ninashukuru kwa uwezeshaji, Sheria na Kanuni zilizowekwa kuwezesha jambo hili.

Tanzania ina imani na mnyororo wa ubadilishanaji wa bidhaa na huduma mipakani na usafirishaji wake kupitia mtandao wa posta. Huduma za posta ni hitaji la msingi kwa watu wote na hutumika kama njia muhimu ya mawasiliano. Vilevile hutumika kama kiunganishi katika biashara mtandao na huduma za TEHAMA. Watoa huduma za posta ni washirika wa kimataifa katika kuunganisha watu na biashara katika maeneo mbalimbali ikiwa ni pamoja na mawasiliano, biashara na ubadilishanaji wa

taarifa na ushauri. Katika kusimamia hili, Serikali kupitia taasisi ya udhibiti, inahakikisha huduma katika Sekta ya Posta zinatolewa bila upendeleo, zenye ufanisi, upatikanaji wa uhakika na salama kwa wananchi wote bila kujali maeneo yao kwa kuzingatia matakwa ya kitaifa.

Maadhimisho ya miaka 150 ya Umoja wa Posta Duniani yanalenga kuonesha mafanikio, fursa pamoja na changamoto katika Sekta ya Posta, si tu kwa UPU kama taasisi ya Kimataifa bali pia kwa Tanzania kama mwanachama wa Umoja huo. Tunaposherehekea maadhimisho haya, tunadhihirisha hatua kubwa iliyopigwa katika kuunganisha teknolojia ya kidijitali katika Sekta ya Posta. Hivyo, Sekta ya Posta haina budi kuendelea kutekeleza majukumu yake katika kuleta mabadiliko kwenye mawasiliano kwa kuruhusu ubunifu na matumizi ya teknolojia ambayo ni muhimu kwa maendeleo endelevu ya kiuchumi na kijamii.

Mabadiliko ya kidijitali yameleta mapinduzi makubwa katika utoaji wa huduma za posta ambapo utaratibu wake umerahisishwa; kupungua kwa muda wa kutoa huduma, usafirishaji na ufikishaji wa barua, vipeto, vifurushi na mizigo; uwezo wa kufuatilia mwenendo wa barua au mizigo pamoja na kuwezesha huduma za kifedha kwa kutumia mifumo ya kidijitali.

Kwa kuhitimisha ujumbe wangu, nisisitize kwamba uwepo wa mifumo ya posta yenye ufanisi na imara katika Mataifa yote ni muhimu kimataifa na pia kwa kila nchi. Maboresho yenye ufanisi na endelevu katika utoaji wa huduma za posta kimataifa yanahitaji ushirikiano wa nchi zote wanachama wa Umoja wa Posta Duniani. Napenda kuchukua fursa hii kuwahakikishia kuwa Tanzania tutashirikiana bila kuchoka na wadau wote kuhakikisha nchi yetu inaendelea kuwa mshirika imara wa UPU.

***Ninawatakia Maadhimisho yenye mafanikio ya Siku ya Posta Duniani, 2024***